

Ushairi wa Abdilatif Abdalla katika Kubainisha Utamaduni wa Waswahili

Joseph Nyehita Maitaria na Richard Makhanu Wafula***

Ikisiri

Makala haya yanafafanua maudhui yaliyomo katika tungo za mashairi ya Abdilatif Abdalla kwa kuzingatia namna masuala ya utamaduni wa Waswahili yanavyowasilishwa. Masuala hayo yanahusu namna wenyeji hao wanavyotangamana na wanavyoshughulikia maisha yao kwa ujumla. Kadhalika, ubainishaji wa vipengele hivyo vimewasilishwa kwa kuzingatia taijriba ya mtunzi kama mmoja katika jamii hiyo. Mashairi hayo yanapozingatiwa, inabainika kuwa: hisi za mtunzi zimedhibitiwa kwa lugha teule ya mafumbo inayojikita katika zaidi katika 'lugha' au 'lafudhi' yake ambayo ni lahaja ya Kimvita. Katika muktadha huu, jumbe hizo zinahitaji fasiri na maelezo kutokana na utamaduni wa mtunzi. Kwa mapana, mashairi hayo yana mwangwi unaogusia historia yataifa lake (hasa katika miaka ya baada ya 1963 nchini Kenya). Kwa maana hii, ushairi wa Abdilatif Abdalla unawenza kwa kihifadhi na kibainishaji cha vielelelzo vya utamaduni na uhalisi wa maisha ya jamii ya mtunzi. Katika kushughulikia uhusiano uliopo kati ya fasihi na utamaduni, makala haya yanaangazia baadhi ya mifano ya mashairi yaliyohifadhiwa katika Diwani ya Sauti ya Dhiki (1973). Mwishowe, inapependekeza namna mashari teule ya Kiswahili yanavyoweza kuwa hifadhi ya 'viashiria' vya 'viishara' vyatamaduni asilia katika jamii ya sasa.

Dhana msingi: *mashairi, Abdilatif Abdalla, utamaduni, Waswahili, mtunzi, lugha, uhalisi, viashiria, viishara*

Abstract

This paper examines the poetry of Abdilatif Abdalla to determine the way in which social cultural issues of the Swahili people are presented. The issues relate to the way in which the people integrate and deal with their life affairs. In addition, the identification of the social cultural issues is based on how the poet, as a member of Swahili society, deals with them. The results show that figurative language, especially the Kimvita dialect, is used to hide the poet's feelings. Therefore, the poet's culture needs to be taken into account in the effort to unravel his messages. Generally, his poetry mirrors the history of his nation (since the years after Kenya's independence in 1963). Thus, the poetry of Abdilatif Abdalla can be a treasure trove of the culture and

* Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Karatina, S.L.P. 10101, Karatina, Kenya, Barua pepe: nyehitam@yahoo.com

** Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, S.L.P. 00100, Nairobi, Kenya, Barua pepe: rnamwinguli@gmail.com

life of his people. In examining the relationship between literature and culture, this paper analyzes some of the poems in the anthology entitled “Diwani ya Sauti ya Dhiki” (1973). Finally, it makes recommendations as to how poems written in Kiswahili can preserve the people’s real culture in the present society.

Key words: poems, Abdilatif Abdalla, culture, the Swahili, poet, language, real, background

Utangulizi

Ushairiwa Kiswahili, kama ilivyo katika tanzu muhimu za fasihi, haziibuki katika ombwe tupu. Hivyo, ni zao halisi la jamii na kupitia kwazo huwa ni nyenzo za kuhifadhi na kuwasilisha utamaduni wa wenyiji⁵. Kimsingi, uwasilishaji huu hupitia jicho la tajiriba na hisi ya watunzi. Kama Iwapo hisia zinazowasilishwa ni za bandia (au si za dhati) hukera na huudhi (Mulokozi, 1999). Kupitia udurusu watungo hizo, hadhira hupata viashiria vinavyohusu itikadi na maono ya mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa utamaduni wa jamii husika. Hivyo, mtunziwa fasihi hususan ushairi wa Kiswahili, huwa na msukumo au kichochococheo kinachomwongoza katika uwasilishaji wa utungo au tungo zake. Hii ndiyo sababu ya kuchukulia kuwa tungo zafasihi ni kioo cha jamii. Katika jamii ya Waswahili⁶, mashairi yamekuwa yakienziwa kamakanzi ya kuhifadhi na kito cha kusawiri na kuelezea masuala muhimu yanayohusu maisha ya wanajamii (Njogu na Chimerah, 1990; Senkoro, 1988). Kumfahamu mtunzi ni kuufahamu utamaduni wa wenyiji uliomlea na kumkuza. Kwa hiyo, kuifahamu jamii inayorejelewa katika tungo hizo nikufahamu ujumbe unaojikita katika muktadha wa utamaduni. Katika jamii ya Waswahili, tungo teule zilitumiwa kubainishia uhalisi wa maisha na pia kuwaelekeza watu kwa kuzingatia utamaduni wao. Isitoshe, ushairi wa Kiswahili katika jamii hii una historia ndefu.

Baadhiya watanzi wanaosifika katika jamii ya Waswahili ni kama vile Ahmed Nassir *Al Inkishafi*, Muyaka wa Hajji *Mashairi ya Muyakana Mwanakupona Utenzi wa Mwanakupona* (Maitaria, 2014; Babusa, 2005). Hapo awali katika jamii ya Waswahili wanaotamakani kwenye upwa wa Afrika mashariki; ushairi wao

⁵ *Utamaduni* unahuusu itikadi, maadili, ishara za jamii, falsafa au uono ulimwengu wa wenyiji kuhusu maisha.

⁶ *Waswahili* ni jamii ambayo inaishi katika upwa wa Afrika Mashariki na lugha yawenyeji ni Kiswahili.

ulikuwa ukitungwa na kuwasilishwa kimasimulizi na baadaye kwa hati za maandishi. Kwa njia ya ubunifu, ushairi katika jamii ya Waswahili umekuwa ni nguzo ya kuusawiri na kuwasilisha uhalisi wa tajiriba yawenyeji kwa kuzingatia jicho la utamaduni wao (Wafula, 2014). Abdilatif Abdalla ni mionganini mwa watunzi watajika katika ulingo wa ushairi huu. Mashairi ambayo amewahi kuyatunga ni kama vile: ‘Napiga Hodi’ katika *Kioo cha Lugha* (1972), ‘Nijile Taka Idhini’na ‘Nishakaribya’ katika Ngurumo (1973) na utenzi wa *Adamu na Hawaa* (1971). Kadhalika, Abdilatif Abdalla aliwahi kuhariri diwani ya ‘*Sikate Tamaa*’ ya S.A. Mohamed (1980) na alishirikiana na Y.Lodhi (1990) katika uhari wa jarida la *Lugha Juzu la 4*. Katika jarida hilo alichangia makala zenyeye mada zifuatazo: ‘Ushairi wa Kiswahili Uhuishwe na Usiuliwe’ na ‘Tanzu za Ushairi wa Kiswahili na Maendeleo Yake’. Kazi ambayo imestasisihishiana kumjengea jina mionganini mwa wahakiki na wasomaji wa fasihi ya Kiswahili, ni mashairi yanayopatikana katika Diwani ya *Sauti ya Dhikambayo* ilichapishwa mwaka wa 1973 na matbaa ya Oxford University Press (K) Ltd. Mashairi hayo yamekuwa ni nembo na pumzi katikakubainishia masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kutokana na mkabala wake na kupitia kwa mawazo yalivyowasilisha katika tungo za mashairi yake, mtunzi huyu anafahamika kama ‘mtoto wa nyumbani’ katika jamii yake. Katika mashairi yake, mtunzi huyu anaweza kuchukuliwa kama msanii aliyesimama kwenye jukwaa huku akitongoa nasaha za kuielekeza jamii na kuitangazia umma mpana kuhusu umuhimu wa utamaduni katika maisha. Kadhalika, usawiri wa ujumbe huo umewasilishwa kwa lugha ya tamathali ilizofundika maono na mielekeo yenye chemchemi iliyojikita katika jamii hiyo.

Mashairi mengi yanayopatikana katika diwani ya *Sauti ya Dhiki yameshughulikia* matukio muhimu ya kihistoria yanayoihusu jamii yake na kwa kiwango fulani, taifa lake la Kenya (hasa katika miaka ya baada ya 1963). Hapa ieleweke kuwa, lugha ya mafumbo katika uwasilishaji wa mashairi hayo, inahitaji fasiriwa mwafaka kwa kuzingatia utamaduni wa jamii yake ya Waswahili uliomzaa, kumlea na kumkuza. Kwa mintaarafu hii, mashairi hayo ni ghala muhimu la kuhifadhia na kubainishia masuala ya utamaduni na uhalisi wa maisha ya Waswahili kama jamii. Kadhalika, ushairi huu unafafanua baadhi ya masuala ya msingi yenyechemchemi yake katika itikadi, imani na maono ya jamii hiyo. Baadhi ya masuala hayo ya kitamaduni ambayo yamebainishwa katika ushairi huo ni kama vile: mahusiano ya wanajamii, uzingativu wa utu, ukarimu, imani, maongozi katika jamii, uhusika wa dhati katika shughuli za

kiuchumi, madhara ya tamaa mionganoni mwa wanajamii, ushirika wa kijamiii na uzingativu wa subira katika kuafikia maamuzi yenyenye mashiko. Maswala hayo pia ni yale ambayo pia yalikuwa yakiangaziwa na watunzi waliotukuka katika jamii hiyo kama vile Mwana Kupona, Ahmed Nassir, Muyaka wa Hajji na Ahmed Nassir (Juma Bhalo).

Kimuundo katika kubainishia masuala muhimu ya kitamaduni katika jamii, mashairi ya Abdilatif Abdalla yanaweza kueleweka katika viwango viwili. Viwango hivyo ni: ubainishaji wa uhalisi wa maisha ya wenyiji na pia kupitia kwa sauti ya shime katika kuielekeza zaidi jamii kuhusu yale yanayopaswa kuzingatiwa ili kujenga ushikamano wa watu katika jamii. Isitoshe, lugha inayotumiwa katika mashairi hayo ni yakiantifora⁷ yenyenye ncha mbili: ya moja kwa moja (au lugha sahili inaeleweka kwa urahisi) na ile ya kiistriari (au ya mafumbo). Kulingana na Olsen (1978), tamathali za usemi hutumiwazaidi katika uwasilishaji watungo za mashairi maarufu. Tamathali hizo ni viashiria-elekezina viashiria-ugwe muhimu vinavyotambuliwa na wenyiji kwa kuzingatiatajriba yao ya maisha na utamaduni. Katika muktadha huu mshairi anayezingatiwa ndiye ugwe unaouunganisha hadhira (wasomaji) na yale yanayoshuhudiwa katika jamii. Katika kushughulikia dhima ya fasihi kama chombo cha kuhifadhia na uwasilishaji wa utamaduni, makala hayayanaangazia baadhi ya mifano katika mashairi yanayopatikana katika Diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973). Mwishowe, inapendekezwa namna ushairi wa Kiswahili unavyowenza kufafanuliwa zaidi kwa malengo ya kubainisha masuala muhimu katika jamii ya sasa.

Muktadha wa Kuibulia Maswali ya Kitamaduni katika Tungo za Kifasihi

Kimsingi, utamaduni katika jamii unahuishisha mirando ambayo kwa pamoja hudhihirisha matarajio, uonoulmwengu na mielekeo ya wenyiji kuhusu maisha. Abdilatif Abdalla ameangazia kwa ubunifu yale yanayotendeka na mabadiliko yaliyopo katika jamii yake kwa uelekezi wa utamaduni wao. Ili kubainisha hayo kuna haja ya kuangazia kauli zilizotumika katika mashairi hayo kama vito (au viishara) vyta kufafanulia hekima na masuala muhimu ya kitamaduni katika jamii yake. Kwa hivyo, ni muhimu kwa msomaji wa mashairi haya kujiuliza maswali yafuatayo:

⁷ Hii ni mbinu ya kitamathali ambapo mtu anajisaili kuhusu yale yanayohusu kisha anayajibu mwenyewe

- a) Nimazingira gani yanayopatikana katika jamii ya mtunzi? Hapa inabainika kuwa ni jamii ambayo inaenzi kilimo cha minazi na jamii hii ni ya pwani.
- b) Ni mambo gani aliyoyashuhudia au yaliyompitikia mtunzi awe na mwelekeo wake kuhusu maisha? Hapa kuna haja ya kuzingatia yale yaliyomtokea kabla ya diwani yake kuchapishwa kama vile athari ya mabadiliko ya maisha na utamaduni wao.
- c) Ni lugha ya aina gani anayoitumia na amefanya uteuzi huo kwa nini? Katika mashairi ya Abdilatifu Abdalla anatumia kauli za Kiswahili wastani na wakati mwingine anapohisi ‘kukereka’ anatumia mafumbo kwa ‘lugha’ yake ya Kimvita.
- d) Mtunzi anawasemeza na kusemezana na akina nani kupitia kwa mashairi yake? Hadhira lengwa katika mashairi ya Abdilatif Abdalla inaweza kugawanyika katika makundi mawili: wenyeji wenyeewe na kwa upana hadhira pana inayopatikana katika taifa lake. Kuna baadhi ya mambo ambayo anayakejeli au yale anayoyapigia upatu?
- e) Kimwelekeo na kihisia, mtunzi ana msimamo ausuluhugani kuhusu yale anayowasilishwa katika mashairi yake? Katika muktadha wa mashairi yake, Abdilatif Abdalla anawataka wenyeji kutathmini upywa mabadiliko yanayojiri katika maisha yao kwa mizani ya utamaduni wao.

Maswali hayo yaliyodokezwa hapo juu yanaweza kufafanuliwa kwa kuzingatia mifano iliyotumika katika maishairi ya Abdilatif Abdalla kama itakavyoelezwa hivi punde. Ingawa wahakiki wa kifasihi wameeleza kuwa mashairi haya ni ya kiharakati na ya kisaiasa; sauti ya utamaduni wa Waswahili pia yanapata nguvu kupitia mifano halisi iliyotumika katika uwasilishaji.

Masuala ya Kitamaduni katika Baadhi ya Mashairi ya Abdilatif Abdalla

Mashairi katika diwani ya *Sauti ya Dhikiyanahusishwa* zaidi na masuala ya kisaisa yaliyowahi kutokea katika historia ya taifa la mtunzi kama inavyodokezwa na baadhi ya wahakiki wa kifasihi (Maitaria, 2014; Chacha, 1992). Hata hivyo, fasiri mwafaka ya mawazo yanazowasilishwa yanaweza kufikiwa kwa kuzingatia uhalisi wa utamaduni wa mtunzi. Miongoni mwa kurunzi za utamaduni wa Waswahili zinazojitokeza katika mashairi ya Abdilatif Abdalla zinafafanuliwa hapa kama ifuatavyo:

Utamaduni Unahusu Mazingira ya Uswahilini

Waswahili kama jamii inapatikana katika upwa wa Afrika ya Mashariki ambapo kuna mandhari ya bahari ya Hindi. Kadhalika, katika janibu hizi kuna minazi ambayo inaenziwa katika maisha ya jamii (Nassir, 1976). Waswahili kama jamii hupenda kuishi vijiji au mashambani, kinyume na mawazo ya baadhi ya watu ambao wamekuwa na mielekeo kwamba, jamii hii nautamaduni wa kupenda maisha ya ‘ubazazi’, anasa na starehe za mjini (Mbaabu, 1985: 3). Kwa mfano, katika shairi la ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’imeelezwa kuwa: *Mnazi yake aswili, uli mbwa wazazi wetu*(uk. 18, ubeti wa 9). Kutokana na uwepo wa mimea hii, wenyeji wana uzoefu wa ukwezi na pia wanafahamu manufaa ya matunda yake kama inavyodokezwa katika shairi lilo hilo kuwa, *Nami nataka kukweya, nitunde nazi hakika* (uk. 19, ubeti wa 15). Kutokana na mandhari na shughuli zinazohusiana na uvuvi na usafiri wa majini, yameashiriwa katika shairi hilo kwamba, *chombo kitakapozama, na kuzama walo ndani* (uk. 21, ubeti wa 31). Chombo hapa ni vile vyombo vinavyotumiwa katika usafiri wa majini kama vile majahazi na meli. Zaidi ya hayo, imeelezwa namna samaki wanavyohusiana majini katika shairi la ‘Mamba’. Kwenye shairi hili kumetumiwa maneno *mamba na mtoni* (uk.10, ubeti wa 2).Hapa ifahamike kuwa, jamii ya Waswahili inafahamu tofauti kati ya mamba na samaki wengine ambao ni wakubwa baharini na mto pia unajulikana. Hata hivyo, kinachorejelewa kwa makusudi hapa ni ‘bahari’ na ‘samaki’wakubwa kama vile papa na nyangumi mionganini mwa wengine. Miktadha ya matumizi ya maneno hayo hayawapi tatizo kwani waelewa mandhari ya pwani, lugha na utamaduni wa Waswahili.

Ushirikiano na Utangamano katika Jamii ya Waswahili

Katika utamaduni wa Waswahili, utangamano wa jamii unachukuliwa kuwa ni wa muhimu sana. Hivyo, watu hushirikiana katika masuala mbalimbali katika kustahiana na kukirimiana wakati wa shida na wakati wa kufurahia maisha wanajamii hujumuika pamoja. Kwa maana hii, dhiki ya mmoja inawahu wote katika jamii. Mwafaka huu umewasilishwa kuititia kwa mahusiano yawalusika wawili: Badi na Alii katika shairi la ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’ (kur. 17-22). Kwa kuwazingatia wahusika hao, mtunzi haoni jambo ambalo linapasa kuyumbisha mahusiano yao ya asili ilhali walielekezwakwa dhati na wavyele wao kabla ya mauko yao. Wavyele hao walitumia kauli za kuwanasihi kuishi katika mahusiano ya kidugu. Zaidi ya nasaha walizozitoa wazee hao, waliwaelekezawana wao kivitendo kuititia namna walivyoishi

kiuduguna kiujirani. Mwafaka huo haukuzingatiwa na mmoja wa wana hao kama inavyodhihirishwa kupitia kwa malumbano yafuatayo:

Alii

Mnazi ni wa shirika, mimi na wewe mwendani
Unshakuwa wataka, kunitowa shirikani?
Hilo halitatendeka, wala haliwezekani
Sikubali abadani (ubeti wa 7)

Mnazi yake aswili, uli mbwa wazazi wetu
Mbwa baba zetu wawili, pasi wa kungiya wa tatu
Mali yao ya halali hawakunyang'anya mtu
Sasa waffle ni wetu (ubeti wa 9)

Badi

Wanambiya nilikuwa, nilikuwa, kilo kichache hikupa
Nami kingi hitukuwa, wananguhenda 'henda kuwapa
Ndiyo sababu wakawa, wanangu wamenenepa
Na nguo njema kuwapa (ubeti wa 24)

Katika madondoo hayo, mshairi anaeleza namna wanajamii walivyokuwa wakiishi pasi na kubaguana na kilichopewa kipaumbele ni kuandama mahusiano mema kulingana na utamaduni wao. Mawazo ya msanii huyu ni kwamba, katika utamaduni wao, mahusiano yasiyofaa katika jamii hayakuwa na nafasi. Hayo yanabainishwa kupitia kwa namna wazazi wa akina Badi na Alii walivyokuwa wakistahiana kidugu na familia hizo mbili ziliandama amani na ushirika katika maisha yao. Mshairi anasikitikia hali ya Badi katika maapuuza ya utamaduni wao wa azali na kuzua uhasidi wa kimahusiano! Hata hivyo, mtunzi anabainisha kiini kikuu cha uhasama huoni kutozingatia maadili kama ulivyobainishwa katika utamaduni wao. Kwamba, tamaa na ubin afsi umewafanya waja kuiga mienendo isiyostahili huku wakisahau misingi ya utu na upendo katika jamii. Kidole cha lawama na shoka la Abdilatif Abdalla linamwangukia Badi ambaye amaekiuka pumzi ya utamaduni wao na mkono wa pongezi unamshukia mhusika Alii kutokana na hulka yake ya kuzingatia utu. Huo ndio mwafaka ambao mtunzi anauhimiza katika shairi hili na kusisitizwa zaidi katika mashairi mengine yanayopatikana katika diwani hii kama vile 'Ah! Mwenzangu'(kur. 29-31), 'Mja si Mwema' (uk. 34), 'Usiniuwe!' (kur. 51-55), 'Sikakawane na Kimya' (kur. 65-66) na 'Kutendana' (kur. 89-110).

Uongozi katika Jamii ya Waswahili

Katika utamaduni wa Waswahili suala la uongozi ni wadhifawa kujukumishwakwajamii. Kiongozi anatarajiwa kujitolea kwa hali na mali ili kuhakikisha wanajamii wanaishi kwa amani na wanatekeleza majukumu yao ya kila siku. Hivyo, kiongozi anatarajiwa kuishi kwa ajili ya wengine au zaidi kuwatumikia wengine katika jamii. Hatarajiwi kuelekezwa kwa mawazo ya binafsi na ubaguzi wa watu katika misingi ya kialila, kinasaba na kiukoo. Alipaswa kuwa mstari wa mbele katika kuhudumia na wala si kutarajia kuhudumiwa katika jamii hii ya Waswahili; watu wote ni sawa. Isitoshe, anahitaji kuwa mtu wa kuridhi kukosolewa na kurekebishwa na wanajamii wenzake. Utamaduni haumruhusu kiongozi kuwa msaliti wa wenzake. Kulingana na jamii hii ya Waswahili, huyu ni mtu wa watu na wala si ‘mungu’ mdogo. Katika utamaduni huu, kila mmoja anahtaji kuwajibika kuhusu masuala ya uongozi. Huu ni uongozi wa kupokezana vijiti kwa awamu na wala haikukubaliwa kiongozi kukatalia kuko huko juu. Endapo wajamii wanahisi kuwa kiongozi wao hatendi yanayostahili huweza kukejeliwa na kukemewaiwapo hatabadili nyendo zake potofu. Hata hivyo, inafahamika kuwa; kukosea kwa mja ni jambo la kibinaadamu na kujirekebishwa ni wajibu na wala si kwa kumdhalilisha au kumvunzia mtu hadhi(Shitemi, 2010). Utamaduni unaohusu masuala ya uongozi yameasilishwa kupitia kwa shairi la ‘Mwerevu Hajinyowi’ (uk. 27). Katika shairi hili, kiongozi ambaye amepokezwa majukumu hayo ya utawala amejawa kiburi cha kujiona ‘ndovu’ na kuwasahau wale waliomkweza. Mshairi hapaanaushutumu ukiukaji wa utamaduni wao kwa kumjulisha kiongozi huyo kuwa:

Tangu ukipate kitu, ’megeuka mpumbavu
Kattu huthamini mtu, ambaye kwamba mtovu
Wafikiri kisu gutu, hakikati nyama pevu?
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe? (ubeti wa 2)

Kupata kusikughururi, ukajidhani mwerevu
Na hicho chako kiburi, ujuwe ni maangavu
Iko siku itajiri, ujikute mwenye wavu
Tangu lini mwerevu, akajijowa mwenyewe? (ubeti wa 4)

Katika beti hizo zilizorejelewa, mshairi anawachukulia viongozi hao kuwa ‘wapumbavu’ na wasiofaa kupewa wadhifa huo kwa kuzingatia vigezo vya utamaduni wao. Kibinadamu, mtu huweza kukosea na inabidi wazee kutoa nasaha kezi (Njogu, 2004) Katika jamii ya

Waswahili, mtu hakatai mawazo kutoka kwa watu wengine. Vilevile, imesawiriwa katika baadhi ya mashairi kuwa, Waswahili ni wataratibuna wapole. Mwenendo huu si msingi wa kufasiriwa kuwa ni wanyonge wa kunyanyawa au kudhulumiwa. Wanahofiazaidi utumiaji wa nguvu unaoweza kuvuruga amani katika jamii. Hata kama kutakuwepo na haja ya kupigania haki yao, utamaduni waounawahimiza kuandama amani kama njia yakurekebishana.. Mfano hapa ni kauli za mhusika Alii katika shairi la la ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’ (kur. 17-22) kama ifuatavyo:

Alii
 Nilitakaloni kuwa, waja wapate yaona
 Wajuwe ’medhulumiwa, kwa muda mrefu sana
 Siku ’kitwaa hatuwa, pamoja na wangu wana
 Pasiwepo wa kunena (ubeti wa 42)

Kupitia kwa dondo hilo inabainishwa kuwa, Waswahili ni watu wenye subira na hawapendi makabiliano yanayotumia nguvu katika kuidai haki yao ila pale wanapohisi kudharauliwa. Mawazo haya pia yanapatikana katika baadhi ya mashairi maarufu ya Waswahili kabla ya karne ya ishirini. Kwa kurejelea Waswahili wa Pate, Muyaka bin Haji(Abdulaziz, 1979)ilitongoa:

Wangwana Pate Yunga, hawatarithia p’ingu.
 Msambe ndiswi wajinga, mututumao kizungu;
 Kwa kibaba cha mpunga, kisichotimia chungu.
 Msikufuruni Mungu, mkangia kufuruni (Abdulaziz, 1979: 122)

Katika dondo hilo Wapate wamesawiriwa kuwa wangwana kwa ambavyo walipenda utu, amani na upendo na katu hawakutaka kudhulumiwa au kuhadaiwa kwa fedha. Mwafaka huu usipozingatiwa, matumizi ya nguvu (ingawa haitarajiji), huwani hatua ya pekee au ya mwisho. Mashairi mengine yanayobainisha mwelekeo huo katika jamii ya Waswahili ni ‘Jipu’(uk.7) ambapo ujumbe wa subira umewasilishwa na ‘Kutendana’ (kur. 89-110) ambapo ukarimu na utu ni baadhi ya masuala yanayosisitizwa zaidi katika utamadni wa Waswahili.

Matumizi ya ‘Lugha’au Lahaja ya Wenyeji

Lugha ni kipengele muhimu cha utamaduni wa jamii. Aghalabu baadhi ya masuala ambayo yamegubikwa katika tamaduni yameashiriwa kwa lahaja au ‘lugha’ ya mzawa. Kwa mfano, Abdilatif

Abdalla anapopandwa hasira na jazba haoni njia nyingine iliyomwafaka zaidi ila kwa kwa kauli zinazojikita zaidi katika Kimvitaambayo ni lahaja yake. Mtindo huu pia unapatikana katika baadhi ya watanzi kama vile Nassir (1971) na Muyaka bin Haji (Abdulaziz, ktj). Ni katika muktadha huu ambapo Abdilatif Abdalla (hata kama anafahamu lahaja nyingine na hata Kiswahili sanifu); anatumia lahaja yake ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe unaotokana na hisi zake. Kadhalika, mshairi huyu amefuma mistari au mishororo katika tungo zake kwa uelekezi wa tajriba yakena kwa lugha ya wenyeji. Anabainisha hisia za ghadhabu na hasira kutokana na yale anayoyashuhudia (Chacha, 1992). Kwa mfano, katika shairi la ‘Siwati’ (uk. 9) sauti ya hamasa na ghadhabu imehanikizwa kupitia kwa lahaja ya Kimvita katika ubeti ufuatao:

Siwati nshishielo, siwati; kwani niwate?
Siwati ni lilo hilo, ’talishika kwa vyovyo
Siwati ni mimi nalo, hapano au popote
Hadi kaburini sote, mimi nalo tufukiwe (ubeti wa 1)

Maneno yaliyopigiwa msitari ni ya lahaja ya Kimvita ili kudhihirishia ukiukaji wa imani inayojikita katika utamaduni wa jamii yake. Suala hili limesisitiwa na limekaririwa kwa neno ‘siwati’ lilitotumiwa mwanzoni mwa mishoro mitatu ya awali. Baadhi ya wahakiki wa fasihi wamekuwa wakishikilia kuwa mashairi hayo ni ya kifungoni naya kuufua moyowake (Maitaria, 2014; Nyanchama, 2004; Chacha, 1992). Ingawa huo ni kweli, kinachosailiwa hapa ni kuwa hisi za ndani za mja huweza kuwasilishwa kwa mwafaka zaidi kwa kuzingatia lugha ya kwanza (Mutonya, 2013). Kwa mantiki hii, utamaduni wa Waswahili unamtaraji mwenyeji kuwa amemakinika katika ‘lugha’ yake. Shairi la ‘Kuno Kunena’ (uk. 23) linafweza kuzingatiwa kama mfano wa kufafanulia zaidi hoja kwamba, utamaduni wa Waswahili wanaienzi ‘lugha’. Kwa kutumia ‘lugha’ yao kwa namna mbalimbali ili kuwasilisha jumbe ambazo zimejikita katika utamaduni wao asilia. Chambilecho mtunzi:

Kuno kunena kwa nini, kunanikomeya kuno?
Kwani kunena kunani, kukashikwa kani vino?
Kani iso na kiini, na kuninuniya mno
Kanama nako kunena, kwaonekana ni kuwi (ubeti wa 1).

Kupitia kwaubeti huo, mtunzi amedhihirisha uzalendo wake katika kuumua ujumi na mahadhi katika uwasilishaji ujumbe wake kupitia kwa lahaja au ‘lugharasmi ya jamii’ yake. Kwa maana hii, mshairi huyu amedhihirisha kuwa; hadhi ya ‘lugha’ yake bado i pale pale na

wala haijatindikiwa kimsimiati katika uwasilishaji wa mchomo wa hisi unaotokana na utamaduni wao. Hivyo, matumizi ya ‘lugha hii’inakuwa ni kiunzicha kusarifu, kuibulia na kukuza hisia kwa kuugotesha ujumbe katika mihimili ya utamaduni wa jamii yake. Hivyo, jumbe katika mashairi ya Abdilatif Abdalla yamewasilishwa pasi na kupotosha maana dhamiriwa.

Ufanyaji Kazi katika Jamii

Utamaduni wa Waswahili unasisitiza haja ya kujituma katika ufanyaji kazi kwa bidii. Kwamba, kazi mtu ana haki ya kufanya kazi na kazi ni uhai. Kulingana na Maitaria (2017), jamii ya Waswahili shughuli za ukulima na upanzi wa minazi ni tegemeo lao kuu ingawa pia kuna baadhi ya watu ambao hubangaiza kupitia kwa biashara. Hivyo, katika jamii ya Waswahili, kazi ni kazi mradi mtu anayayasuma maisha yake na ya familia. Masuala hayo yamedokezwa katika baadhi ya mashairi yanayopatikana katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Kwa mfano, katika shairi la ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’ (kur. 17-22) mhusika Alii hapati nafasi ya kushiriki kwa dhati katika ufanyaji kazi kutokana na kuondolewa au kubaguliwa katika shughuli hii muhimu kama anavyolalamikia hali hiyo, kwamba:

Alii
 Sababu ya kukwambiya, ya kwamba ushuke tini
 Ni kuwa nataka kweya, huko juu mnazini
 Kwa ajili nami piya, nitunde nazi mwendani
 N’shakueleza kwa nini(ubeti wa 3)

Kadhalika, mawazo yanayowasilishwa katika ubeti huo kuhusu kazi yameendelezwa pia katika shairi la ‘Zindukani’ (kur. 69-72) ambapo mshairi anaisihi jamii kuzingatia maelekezo ya utamaduni wao kuhusu umuhimu wa kufanya kazi katika jamii. Kwamba, utamaduni wao hauruhusu kutarajia majaliwa na kusubiri kufanyiwa. Hivyo, mshairi ambaye ni mwanajamii, anachukizwa na mielekeo ya baadhi ya watu kuhusu kazi. Baadhi ya watu wamekuwa wakiendekeza uvivu na starehe kwa kuhofia kutoa jasho katika kazi za sulubu kama inavyoelezwa katika ubeti ufuatao:

Muzowele kubwagaza, na kungoja majaliwa
Viingo mumviviza, hamtaki jisumbuwa
 Hamuna munaloweza, mwataka ya kufanyiwa
 Daima tutapwelewa, jamani amshanani (ubeti wa 2)

Katika muktadha wa ubeti huo, mashairi amebainisha kuwa, kazi ni muhimu ili kuweza kuheshimiwa katika jamii. Kutegemea vyta bure na uzururaji katika jamii ya Waswahili ni jambo la kuudunisha utu wa mtu. Uzembe katika jamii umekuwa ukikemewa kupertia kwa kauli anazozitoa mtunzi katika mashairi yake. Mawazo hayo pia yamewasilishwa katika shairi la ‘Kutendana’ (kur. 89-110).

Uzingatiaji wa Haki katika Jamii

Kamwe Waswahili hawapendi kuhiniwa haki yao; iwe kwa ulaghai wa wazi au kwa siri. Wanachoamini ni kuwa, haki ya mja haizami. Mifano ipo ya kuwaelekeza watu dhidi ya tamaa na kutotenda haki. Katika jamii ya Waswahili kuna methali kama vile ‘Mtaka vingi kwa pupa hana mwisho mwema’, ‘Mtaka yote hukosa yote’ na ‘Mui muuwe na haki yake uumpe’ (Wamitila, 2001). Methali hizo ni viashiria vyta uhalisi wa utamaduni wa Kiswahili na hutumika kuwahimiza watu kutoelekezwa kwa tamaa na kielekezo ni kutenda mema. Utamaduni wa jamii Waswahili unawaelekeza watu kuzingatia utu, ukarimu na kutokuwa na chukimiongoni mwao (Shitemi, 2010). Aidha, katika jamii ya Waswahili, watu ambao hupenda haki kutendeka, kupata stahiki yao nawala hawakubali kurubuniwa katika maisha yao. Aidha, wanaanini kuwa mtenda maovu katika jamii hadumu na malipo ya ubaya ni papa hapa duniani. Kwayule anayetenda wema ni kama ‘anajiwekezea’ na kijijengea jina kwa Mwenyezi Mungu. Kwa yule anayekiuka mwafaka huo inachukuliwa kuwa, adhabu kali kutoka kwa Mungu itamshukia. Katika masuala hayo yanayohitaji haki kutendeka katika jamii ni moja tu: kumpa mja haki yake na wala si yenye walakini. Hakuna vishawishi ambavyo vinaweza kulegeza misimmo yao kama inavyoelezwa ifuatavyo katika shairi la ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’ (kur. 17-22):

Alii

Pamoja tulipokuwa, vyetu tuvitanganya
Jambo moja hagunduwa, ulokuwa ukifanya
Hukuwa kinipa sawa, wakati wa kugawanya
Changu ukinipokonya (ubeti wa 21)

Badi

Uliona ni vizuri, kichache kutokubali
Ukafanya nyingi ari, ya kukiwata kalili
Ni heri nusu ya shari, kuliko shari kamili
Au hufahamu hili? (ubeti wa 26)

Katika malumbano hayo ya Alii na Badi kuna jambo ambalo linadhihirika kuhusu utamaduni wa Waswahili: kwamba, haki ya mtu haihitaji kuporwa au kufanyiwa udanganyifu. Kwa mfano Alii anashangazwa na vitimbi vya mwenzake ambapo anatumia ujanja katika kumhini halali yake. Hivyo, Alii anakataa kuchukua fungu ambalo si kamili na pia hataki kupewa vijizawadi vya kumfumba macho kwa stahili yake. Kutokana na utamaduni wao, dhamiri ya Alii inamwonya dhidi ya kutenda mambo ambayo yatamvunja staha yake katika jamii. Utu wa mtu ni kuitunza heshima yake binafsi na pia kuhakikisha kuwa jina lake halichafuliwi katika jamii. Wanajamii wanafahamu kuwa tendo jema halishauliki. Katika muktadha huu, Alii hataki kabisa kujihusisa na maswala ya kisiri siri, kwa sababu mambo hayo huweza kutibuka na ikawa izara kwake. Hii ndiyo maana ya mshairi kushilia kuwa, haki ya mja sharti itetewe kwa gharama yoyote. Hili linadokezwa katika shairi la ‘Siwati’ (uk. 9) ambapo mshairi ana msimamo mkali katika kukataa ushawishi wa aina yoyote utetezi wa hakikama inavyosawiriwa hapa:

Siwati si ushindani, mukasema nashindana
 Siwati ifahamuni, sababuye waungwana
 Siwati ndangu imani, niithaminiyo sana
 Na kuiwata naona, itakuwa ni muhali (ubeti wa 3)

Katika beti hizo zilizonukuliwa, imedhihirishwa msimamo wa utamaduni wa Waswahili kuhusu utetezi wa haki pindi inapohatarishwa.

Kuhusu Rasilmali ya Jamii

Jamii ya Waswahili hutegemea kilimo cha mnazi kama uti wa mgongo wa uchumi wao. Hii ni mali ya umma na inatarajiwa kuwafaidi wote katika jamii. Kutokana na mazingira ya ukuwa baarini, Waswahili pia wanajishugulisha na uvuvi. Hata hivyo, kuna baadhi ya watukama vile mabepari, manweyenye na makabaila (ambao wamekiuka mwafaka huo kwa uchu wa kujitajirisha wao wenye kwa kuhodhi mashamba na minazi iliyopo. Kulingana na utamaduni wa Waswahili, wanaoihodhi minazi kukidhi haja zao za kibnafsi huchululiwa kuwa ni wezi na majambazi. Kwa mfano, Badi amezua mbinu za kughushi umilishi wa mnazi uliorithishwa na wavyele wao kabla ya mauko. Katika muktadha huu, wale waliokosa hudoda na kuogelea katika ultima na umasikini. Mazingira haya yanaisukuma na kuwabandua wanajamii kutoka kwa uelekezi wa uutamaduni wao ambapo

migawanyiko ya kitabaka haikuwepo (Imbosa, 1990). Kuna uwezekano wa baadhi ya watu hawa kuwa wameathiriwa na utamaduni wa kigeni kutokana na mtagusano wa watu. Athari hizo ndizo zinazopigwa darubini na mshairi huyu katika shairi la Mnazi: Vuta N'kuvute' (kur. 17-22) kwamba:

Alii
Walipoaga duniya, kuenenda kwao kuzimu
Mnazi waliit'watiya, baba zetu waadham
Tuurithi sote pia, ili tusiwalaumu
Je, unshafahamu? (ubeti wa 12)

Katika ubeti huo, Alii anarejelea namna wazee wao walivyokuwa wanawatakia amani katika mahusiano yao ya siku zijazo kama walivokuwa wakiishi katika jamii. Hata hivyo, kwa ufidhulina kiburi kinachoelekezwa kwa tamaa ya ubinafsi Badi (ambaye ni mwenzive Alii) tayari amezugika akili na kutaka kuuhodhi mnazi na nazi zake; hasikii wala haambiziki. Iburi hicho cha Badi imeelezwa hapa:

Badi
Makosa haya si yangu, ya wanayo kudhikika
Lau hilo dogo fungu, kwako ungaridhika
Watoto wako ndu yangu, wasingetaabika
Bali hili hukutaka (ubeti wa 25)

Kulingana na mawazo ya mshairi, kutozingatia utamaduni asilia katika jamii ndio unaosababisha kuwepo kwa mgaragazo na kuwafanya watu katika jamii kuwekwa katika matapo ya kidhahania yanayoundwa kwa utashi wa tamaa ya kujilimbikizia utajiri na kujiona bora kuliko wengine katika jamii. Tangu azali wanajamii hawakupasa kukosa lishe iwapo baadhi yao wana walichokisaza. Isitoshe, utu ulithaminiwa zaidi kuliko utajiri alionao mtu.

Hivyo, ujanja wa kibinafsi unaotumika katika uporaji au ukosefu wa mnazi na mazao yake ndio chechemi ya uhitaji, ukata, chochole na umaskwota katika jamii hii inayosawiriwa na msanii. Hivyo, walalahai na walalahoiUswahilini ni jambo ambalo limechongwa na baadhi ya watu wachache na wala si najaliwa. Matokeo ya hali hii ni chemchemi ya kuubomoa mshikamano katika jamii ya Waswahili. Haya ni mambo ambayo yanabainishwa na Alii (kama ilivyoelezwa hapa juu) ambaye zaidi ya kuwa kielelezo cha mja anayetafunwa kwa ukata unaosababishwa na mja mwenzake;ni kikuza sauti cha

mtunzi katika kuupitisha ujumbe unaojikita katika utamaduni wa jamii yake. Msanii huyu analimwaya dukuduku lake linalomsakama moyoni kuhusu fadhaa inayhusu ukiukaji wa taratibu za mila na desturi ya Waswahili. Kukirihishwa kwake kunajitokeza kupitia kwa kauli zinazotumiwa na Alii ambaye anashangaa kinachomtia kiwi Badi (baadhi ya wanajamii) ambaye anakosa kuuona mwafaka uliojengwa nawavyele wao. Kuingana na mtunzi ni kwamba watu kama hawa (akina Badi) wanahitaji kuondolewa na kutupwa pembeni. Ukiukaji huu unajenga tuhuma, chuki na kuinjikiana visasi ambapo haikupasa kuwepo katika utamaduni wao. Raslimali ya jamii inahitaji kulindwa na kuhifadhiwa kwa maufaa ya kizazi kilicopo na kijacho. Mashairi mengine yenye mwelekeo kama huo ni ‘Mamba’ (uk. 10), ‘Usiniuze!’ (kur. 51-55) na ‘Kutendana’ (kur. 89-110).

Masuala mengine Yanayohusu Utamaduni katika Mashairi ya Abdilatif Abdalla

Masuala ya kitamaduni yaliyofafanuliwa hapo juu siyo ya pekee yanayojitokeza katika mashairi ya Abdilatif Abdalla. Kuna mengi ambayo yanaweza pia kuhusishwa kuutambua zaidi utamaduni wa Waswahili. Hapa yametajwa baadhi ya masuala hayo ambayo pia ni muhmu. Itikadi na imani katika jamii ya Waswahili (baadhi ya mambo hayo ni kama vile: mashetani, pepo na dini) inajitokeza kwa namna jamii inavyomtegemea Mungu katika masuala yanayohusu maisha ya watu (Wafula, 2014). Suala hili linawenza kufafanuliwa kwa kuzingatia namna anavyotumia nafsi ya kwanza katika kauli zake huku akisemezanana moyo wake na kuwasemeza wanajamii katika mashairi yafuatayo: ‘Tuza Moyo’ (uk. 6), ‘Yatakoma’ (uk. 28); ‘Jana na Leo na kesho’ (kur. 42-46); ‘Moyo Iwa na Subira’ (kur. 48-50) na ‘Kutendana’, (kur. 89-110). Kuhusu mahusiano ya wazee kwa vijana, kuna uelekezo kwamba wazee wana jukumu la kuwaelekeza vijana kuhusu maisha. Vijana nao wanahitajika kuwatiina kuwaheshimu wazee wao kwa kila hali. Haya yamedokezwa katika mashairi: ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’ (kur. 17-22), ‘Usiniuze!’ (kur. 51-55). Tamaa na ubinafsi ni baadhi ya mambo ambayo hayana nafasi katika utamaduni wa Waswahili. Haya ni mambo ambayo humpunguzia hadhi mja na pia kusababsha mahusiano mabaya katika jamii kama inavyobainishwa katika mashairi: ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’ (kur. 17-22) na ‘Kutendana’, (kur. 89-110) na ‘Mamba’ (uk. 10).

Kuhusu ndoa na majukumu yake katika jamii ya Waswahili ni kwamba, mume ndiye anayetarajiwa kuiongoza na kukidhi mahitaji

ya familiayake (Momanyi, 1998). Haki ya watoto katika familia imezingatiwa katika utamaduni wa jamii. Aidha, Mwanamke pia anaweza kuchangiakatika kuikimu familia yaoiwapo mumewe ameshindwa katika majukumu ya kifamilia. Hapa ifahamike kuwa, mwanamke katika ndoa ana majukumu mengine ambayo ni ya muhimu lakini si ya nje ya boma. Mwanamke anaweza kufanya kazi hizo za ‘mwanamume’ endapo mume ni mgonjwa au amekumbwa na baa fulani kama inavyoolezwa katika mashairi: ‘Kamliwaze’ (uk. 5), ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’ (kur. 17-22) na ‘Kutendana’ (kur. 89-110). Waswahili ni wataratibu na wala hawana papara katika yale wayatendayo, huwa na subira kwa kuhofia hasara inayoweza kutokana na ukosefu wa kutokuwa makini au kuzingatia haraka katika maisha. Haya yamedokezwa katika mashairi: ‘Jipu’(uk. 7), ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’ (kur. 17-22), ‘Yatakoma’ (uk.28), ‘Moyo Iwa na Subira’ (kur. 40-49) na ‘Kutendana (kur. 89-110). Sula la uigaji wa utamaduni kutoka nje ya jamii unahitaji udhibtiwa kwa sababu unavuruga misingi ambayo imekuwa ni mihimili muhimu katika uelekezaji wa maisha ya wenyeji. Kwa maono ya mshairi utamaduni huo wanje tayari umeanza kuzinyemelea na kuzivamia taasisi ‘takatifu’ katika jamii hii kama vile ubinagsi, ubwanyeye, ukabaila na vijana kukosa kutii maelekezo ya wavyele wao. Haya yanabainishwa katika mashairi: ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’ (kur. 17-22), ‘Kutendana, (kur. 89-110) na ‘Ah! Mwenzangu’(kur. 29-31). Kadhalika, katika jamii ya Waswahili watu wana uhuru wa kutoa mawazo na kusema yaliyo moyoni bila kificho. Hawaoni raha hadi pale wameyatoa hadharani au kwa yule anayekusudiwa.Hivyo, kuzinduana na kuelekezana katika jamii ni mambo la muhimu mno: hata kama jambo fulani linachoma, huelezwa kwa pumzi yiyo hiyo.kwamba, ukweli ni ukweli hata kama hakuna anayesema ukweli.Kulingana na utamaduni wa jamii hii ni kwamba, hawataki kunong’ona ila la kweli husemwa hadharani kama inaonakidiwa katika mashairi: ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’ (kur. 17-22), ‘Mwerevu Hajinyowi’ (uk. 27), “Sikakawane na Kimya’ (kur. 65-66) na ‘Kutendana’ (kur. 89-110).

Hitimisho

Makala haya yamefafanua namna suala la utamaduni liliyyobainishwa katika baadhi ya mashiri ya Abdilatif Abdalla.Kihalisia, mtunzi amechota baadhi ya mambo muhimu yanayoihusu jamii yake na pia kwa kuzingatia vipengele vya kihistoria. Kiubunifu, mtunzi huyu ameutumia ushairi kama chombo cha kuwasilishia tajiriba yake katika jamii. Kupitia kwamashairi yake, mtunzi huyu amejibainisha kama mhifadhi wa

historia na mlezi wa utamaduni wa wa jamii yake. Katika misingi hiyo, ushairi wa Abdilatif Abdalla unakuwa ni kioo cha kubainishia tajiriba ya watu kuhusu uhalisi wa maisha unaojikita katika utamaduni wao. Ingawa kwa wakati wa sasa kuna mabadiliko tumbi tumbi yanayoshuhudiwa katika maisha ya watu, mshairi huyu ameashiria namna jamii za sasa zinavyoweza kuhifadhi utamaduni wao kifasihi. Hivyo, ujumbe unaowasilishwa kupidia kwa kauli teule ambazo ni vitomeo vya hekima katika mashairi hayo huweza kufasiriwa kwa mwafaka kwa kuzingatia utamaduni uliomzaa, kumlea na kumkuza mtunzi. Hii ichukuliwe kuwa nihatua ya awali ya ubunguaji bongo kabla ya ujumbe huo haujatanuliwa kiufasiri na kupatanishwa kimuktadha na masuala muhimu yenyе mshabaha huo katika jamii anuwai za Afrika Mashariki na kwengineko. Hili litahakikisha kuwa, utamaduni wa asili wa wenyeji haudidimii na hadhi yake itaendelea kuwepo katika mabadiliko yanayojiri katika jamii za sasa. Ndoto ya Abdilatif Abdalla (na nii ni ku;pitia kwa mashairi yake), ni kwamba, jamii za Afrika zina utajiri mkubwa kwa kuzingatia unuwai wa tamaduni zake. Kwa mintaarafu hii, jamii za sasa hata ingawa zimeathiriwa namabadiliko katika maisha; zinahitaji kupata suluhu siyo kwa mtazamo nje bali kupidia kwa uelekezi na mtazamo wa tamaduni asilia. Ndoto hiyo inahitaji kuchochéokupitia kwa tajiriba za wenyeji kwa manufaa ya kizazi cha sasa na cha baaadaye. Aidha, utafiti zaidi uelekezwe kwa ufasiri mashairi ya mashairi ya Abdilatif Abdalla kwa kuhusisha mtazamo pana wa Afrika Mashariki. Katika kufanya hivyo, itasaidia katika kufafanua zaidi mtindo wa uwasilishaji na dhima ya ushairi katika kuchangia ustawishaji wa msamiati wa Kiswahili kwa sasa. Kutokana namazingira hayo, falsafa ya Waswahili kuhusu maisha itadhihirika zaidi kupidia ushairi wa Kiswahili.

Marejeleo

- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.
- Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka 19th Century Swahili Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Chacha, C. N. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya Utetezi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Imbosa, R. (1990). Jazanda katika Ushairi wa Muyaka. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Khatib, M. S. (1999). Tamathali za Usemi. *MULIKA Juzu, 25*. Dar es Salaam: TUKI.

- Maitaria, J. N. (2014). Dhima ya Ushairi wa Kiswahili katika Kuelimishia jamii kuhusu Demokrasia. *KISWAHILI Juzu*, 77. Dar es Salaam: TATAKI.
- Maitaria, J. N. (2017). Ushairi kama Chombo cha Kuhifadhia na Kuelimishia Jamii kuhusu Utamaduni: Mfano wa Mashairi Yanayotumia Methali. Katika M. Kandagor, N. Ogechi & C. Vieke (wah.). *Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja*. Eldoret: Moi University Press.
- Maitaria, J. N. (2018). Ushairi wa Muyaka kama Chombo cha Kubainishia Historia ya Waswahilii. Katika Mwita, L. C. na Wenzake (wah.). *Isimu na Fasihi ya Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.
- Masinde, E. (2003). Ushairi wa Kiswahili na Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui. Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Nairobi: Publishing and Book Marketing.
- Momanyi, C. (1998). Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika Jamii ya Waswahili kama Inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Mulokozi, M. M. (1999). *Tanzu Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mutonya, M. (2013). *The Politics of Everyday Life in Gikuyu Popular Music in Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications.
- Nassir, A. (1976). *Malenga wa Mvita*. Nairobi: Oxford University Press.
- Njogu, K. & Chimerah, R. (1990). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K. (1993). Dialogic Poetry: Contestation and Social Challenge in East African Poetic Genres. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Yale. (Haijachapishwa).
- Njogu, K. (2004). *Reading Poetry as Dialogue*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyanchama, M. B. (2004). Matumizi ya Taswira na Istiara katika *Sauti ya Dhiki*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Olsen, H. S. (1978). *The Structure of Literary Understanding*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Shitemi, N. L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini*. Eldoret: Moi University Press.

- Wafula, R. M. (2014). Nadharia za Uhakiki Kama Mchakato wa Kutaalamisha Usomaji wa Fasihi. *Journal of Linguistics and Language in Education.*
- Wamitila, K. W. (2001). *Kamusi ya Methali za Kiswahili*. Nairobi: Longhorn.